**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. STERGOMENA LAWRENCE TAX (MB.), WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA AKIWASILISHA BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 kwa Fungu 57: Wizara, Fungu 38: NGOME, na Fungu 39: JKT na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana wakati Nchi yetu ikiwa katika hali ya amani, utulivu, na usalama.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumpongeza sana **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuchaguliwa

kuwa Mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar kuwa Mgombea urais wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu ujao utakaofanyika mwezi Oktoba 2025. Kuchaguliwa kwao ni kielelezo cha imani kubwa waliyonayo wana CCM kwa viongozi hawa, kutokana na uongozi wao mahiri na imara unaozingatia maslahi ya Taifa. Nitumie nafasi hii kuwaomba watanzania wote kuendelea kuwaunga mkono, kwa mustakabali wa maendeleo ya Nchi yetu.

*4.* ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii pia, kumpongeza **Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, Katibu Mkuu wa CCM kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu ujao. **Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi** ni mwanadiplomasia na mwanasiasa mkongwe mwenye uzoefu mkubwa ndani ya Chama cha Mapinduzi, na jumuiya za kimataifa.

5. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua kuwa huu ni Mkutano wa mwisho wa Bunge hili kabla ya Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba 2025, kwa unyenyekevu mkubwa namshukuru kwa dhati **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge mwezi Septemba 2021 na kuniteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mara mbili, nikiwa mwanamke wa kwanza katika historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

tangu kupata uhuru. Hii ni heshima, kwangu na wanawake wote wa kitanzania, na dhamana kubwa, ambayo nitaienzi siku zote za maisha yangu. Aidha, ninamshukuru pia kwa kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kipindi cha uongozi wake. Pia, namshukuru kwa kuendelea kuwaamini **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe,** kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na **Jenerali Jacob John Mkunda,** kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, nampongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa jitihada zake za dhati za kuimarisha Wizara ya Ulinzi na JKT, na hivyo kuliimarisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na amani, imara na lenye utulivu na mshikamano. Vilevile, napenda kuwashukuru **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na **Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.)**, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao makini, na kwa miongozo mbalimbali wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ninayoisimamia.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi **Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)** kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na viwango vya hali ya juu. Vilevile, nampongeza **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.),** Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa umakini na weledi. Pia, nawashukuru Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mnadhimu Mkuu na watendaji wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na **Mhe. Vita Rashid Kawawa (Mb.),** akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti **Mhe. Vincent Paul Mbogo (Mb.),** pamoja na wajumbe wa Kamati, kwa maoni na ushauri wanaoendelea kutupatia, ikiwa ni pamoja na katika maandalizi ya Bajeti hii. Maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati wakati wakichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, na mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, yamesaidia kuboresha mapendekezo ya makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, ninayoiwasilisha leo hapa Bungeni.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu na Taifa kwa kuondokewa na **Hayati David Cleopa Msuya** aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu, **Marehemu Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile** aliyekuwa Mbunge wa Kigamboni, na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kanda ya Afrika, **Marehemu Profesa Philemon Sarungi** aliyewahi kutumikia Taifa letu kwa nafasi ya Mbunge, Mkuu wa Mkoa na Waziri katika Wizara mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Ulinzi na JKT, **Marehemu Jaji Fredrick Mwita Werema** aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, **Marehemu Balozi Juma Volter Mwapachu** aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na **Marehemu Bibi Sifael Mushi** Mwanamke aliyeshiriki katika tukio la kuchanganya udongo wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar**.** Napenda kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, na Watanzania wote kwa kuondokewa na viongozi hao.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia fursa hii kutoa pole kwa Amiri Jeshi Mkuu, familia, ndugu na jamaa kufuatia kifo cha **Jenerali David Bugozi Musuguri (Mstaafu)** aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Tatu kuanzia Mwaka 1980 hadi 1988, kifo cha **Meja Jenerali Martin Shiminzi Busungu (Mstaafu)** aliyewahi kuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Kuanzia Mwaka 2018 hadi 2019, kifo cha **Meja Jenerali Charles Mang'ela Mbuge (Mstaafu)**

aliyewahi kuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Kuanzia Mwaka 2019 hadi 2021 na vifo vya wanajeshi waliopoteza maisha kupitia misheni za Ulinzi wa Amani wakati wakipigania amani katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

11. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua kuwa mwezi Oktoba 2025 kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa kumchagua Rais, Wabunge na Madiwani. Vilevile, kwa kuzingatia kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, naomba kutoa rai kwa watanzania wote kujitokeza na kutimiza wajibu wao wa kikatiba, na kutumia haki yao ya kuchagua viongozi sahihi watakaoendelea kuwaletea maendeleo pamoja na kudumisha ulinzi, amani, utulivu na usalama. Niwatakie kila la kheri wote watakaogombea nafasi hizo.

## B. HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

12. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/25, hali ya mipaka ya Nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilomita **5,923.41,** ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji, imeendelea kuwa shwari. Mipaka hiyo ya nchi kavu ni baina ya Tanzania na Burundi, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda, Zambia na mipaka ya Bahari ya Hindi inayojumuisha nchi za Comoros na Shelisheli. Katika kipindi husika hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina yetu na nchi tunazopakana nazo, mbali na changamoto kadhaa za ulinzi na usalama.

### Mpaka wa Tanzania na Burundi

13. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **468.85** ni shwari. Hakuna matukio yoyote yaliyoripotiwa kuhatarisha usalama, ingawa eneo hili linakabiliwa na uwepo wa uharibifu wa alama za mipakani, wahamiaji haramu, uvamizi wa wakulima na uingizaji wa mifugo kwa ajili ya kupata malisho. JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Usalama limeendelea kukabiliana na hali hii.

**Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **554** ni shwari. Hata hivyo, ndani ya Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo waasi wameshambulia na kuiteka miji ya Goma, Sake na Bukavu iliyopo mashariki mwa Nchi hiyo. Wizara kupitia JWTZ imeendelea kuwa macho na kujipanga wakati wote. Katika maamuzi ya vikao vya Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu kutatua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu nchini DRC, walisisitiza umuhimu wa kutafuta suluhisho la kudumu kupitia njia za majadiliano. Aidha, kufuatia uamuzi huu Wakuu wa nchi za SADC walifikia uamuzi wa kuondoa vikundi vya Kijeshi vya SADC nchini DRC, ili kupisha michakato ya kisiasa na majadiliano. Aidha, ushiriki wa Tanzania kupitia Misheni ya Umoja wa Mataifa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*United Nations Organisation Stabilization Mission in the Democratic Republic of the Congo – MONUSCO*), unachangia katika kuleta amani katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Nchi yetu kujiimarisha kiulinzi ipasavyo.

**Mpaka wa Tanzania na Kenya**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **1,187** ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama dhidi ya Tanzania lililoripotiwa. Hata hivyo, ipo changamoto ya uharibifu wa alama za Mpaka. Kazi ya kuimarisha Alama za Mpaka huu inayotekelezwa na Timu ya wataalam kutoka Tanzania na Kenya inaendelea vizuri.

**Mpaka wa Tanzania na Malawi**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama ya Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **394**, ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama lililoripotiwa. Ushirikiano uliopo baina ya Jeshi letu na Jeshi la Malawi ni mzuri. Changamoto ya Mpaka katika Ziwa Nyasa inaendelea kufanyiwa kazi kupitia Tume Maalum ya Usuluhishi (High Level Mediation Team) iliyoundwa na Jopo la Viongozi Wastaafu wa Afrika (African Leadership Forum). Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kupata ufumbuzi kuhusu suala hilo.

**Mpaka wa Tanzania na Msumbiji**

17. ***Mheshimiwa Spika*****,** hali ya usalama wa Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **922.76**, haitabiriki kutokana na uwepo wa Kikundi cha kigaidi cha **Ansar Al Sunna Wal Jamaah (ASWJ)** maeneo ya Kaskazini mwa Msumbiji, katika Jimbo la Cabo Delgado linalopakana na Mkoa wa Mtwara. Kikundi hicho kimekuwa kikiathiri usalama kwa kuendelea na harakati za kigaidi, ikiwemo kulingania wapiganaji wapya kujiunga na kikundi hicho. Hali hii imedhibitiwa kwa kiasi kikubwa, na JWTZ imeendelea kuimarisha ulinzi mpakani kwa kufanya operesheni za ndani ya Nchi kukabiliana na Kikundi hicho, kwa kushirikiana na Jeshi la Msumbiji. Operesheni hizi zimeendelea kuimarisha ulinzi katika eneo la Mpaka, kudumisha amani na utulivu.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuwa operesheni zimesaidia kupunguza nguvu ya Kundi hilo la kigaidi, bado linafanya mashambulizi kwa kuhamahama na kubadili mbinu za kimapigano. Vikundi vyetu vinaendelea kupambana kuhakikisha Kundi hilo halileti madhara zaidi. Wizara inaishukuru Serikali, hususan **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kulipa kipaumbele suala hili, ikiwa ni pamoja na kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa zana na mahitaji mbalimbali yanayosaidia vikundi vyetu kupambana na Kundi hilo.

**Mpaka wa Tanzania na Rwanda**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **230** ni shwari, ingawa yapo matukio machache ya kihalifu yanayofanywa na wahamiaji haramu na uingizaji wa mifugo kwa ajili ya malisho. Wizara kupitia JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Usalama inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti matukio hayo.

**Mpaka wa Tanzania na Uganda**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **397.80** ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa Nchi yetu. Pamoja na hali hii, kumekuwepo na tishio la kiusalama linalotokana na Mgogoro wa Mpaka Kati ya Tanzania na Uganda. Pamoja na jitihada za kumaliza mgogoro huu, bado Serikali ya Uganda inaendelea kudai kuwa mpaka wake na Tanzania katika eneo la Kagera unapita katika $01^0$ Kusini mwa Ikweta badala ya marundo ya mawe yaliyopo. Mazungumzo yanaendelea chini ya uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushughulikia suala hili.

**Mpaka wa Tanzania na Zambia**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika Mpaka huu wenye urefu wa kilomita **345**, ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa Nchi yetu lililoripotiwa hadi sasa.

**Mpaka Katika Bahari ya Hindi**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu wenye urefu wa *Nautical Miles* **864.376** sawa na kilomita **1,424** ni shwari. Katika Mpaka huu tumepakana na Nchi za Comoros na Shelisheli**.** Hakuna tukio lililoripotiwa la kuhatarisha usalama dhidi ya Nchi yetu. Aidha, JWTZ imeendelea kufanya doria za mara kwa mara katika eneo la Bahari ya Hindi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama ili kubaini na kuzuia uharamia, wahamiaji haramu, uvuvi haramu, usafirishaji haramu wa binadamu, usafirishaji wa dawa za kulevya na matishio ya kigaidi.

**Ulinzi na Usalama wa Anga la Juu**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama wa Anga la Juu ni shwari, ingawa kumekuwa na hali isiyotabirika kutokana na kuongezeka kwa matumizi za teknolojia ya kisasa. Aidha, Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi nyingine inaendelea kujiimarisha kwa vifaa, zana, wataalam, mafunzo na semina, lengo likiwa ni kuhakikisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakuwa salama dhidi ya matishio ya Anga la Juu.

## C. UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika kikao cha Bunge cha 13 kilichofanyika Februari 2025, katika Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi, na Usalama. Kamati iliridhika na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio hayo. Aidha, tarehe 20 Machi, 2025 Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26. Kamati ilitoa maoni, ushauri na maelekezo yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Napenda kuishukuru Kamati na kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa, wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

## D. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) 2020 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara imeendelea kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 kwa masuala yaliyoainishwa kwenye **Sura ya Tano** Ibara ya 105 ya Ilani yanayohusiana na Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni:

a. *Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake ili kudumisha Muungano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, umoja, mshikamano, amani na usalama wa raia na mali zao;*

b. *Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;*

c. *Kuwezesha ushirikiano wa vyombo vya ulinzi na usalama kufanya utafiti na ubunifu kwa kushirikiana na taasisi za utafiti;*

d. *Kuhusisha kikamilifu Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati;*

e. *Kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Akiba na ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;*

*f.* *Kuimarisha uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kushiriki shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda katika sekta ya ulinzi na maeneo mengine ya kimkakati;*

*g.* *Kuimarisha viwanda vya NYUMBU na Mzinga ili viweze kutimiza azma ya kuanzishwa kwake;*

*h.* *Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi;*

*i.* *Kupanua na kuongeza idadi ya kambi za JKT na JKU ili kuwezesha vijana wengi zaidi wakiwemo wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya mafunzo ili kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea; na*

*j.* *Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia makazi bora na kuongezea uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia mafunzo ya kitaaluma na kitaalam, vitendea kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa.*

26. ***Mheshimiwa Spika***, maelekezo haya ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 yameendelea kujumuishwa katika Mipango na Bajeti ya Wizara kila Mwaka kama inavyoonekana katika sehemu ya mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, masuala yote haya yamezingatiwa katika mipango ya Wizara na taasisi zake.

## E. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

### Tathmini ya Makusanyo ya Maduhuli

27. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu yafuatayo: Fungu 38: NGOME **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39: JKT, **Shilingi 64,403,000.00,** na Fungu 57: Wizara **Shilingi 1,200,000.00**.

28. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili 2025, Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 178,759,103.08** sawa na **asilimia 204.06** ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38: NGOME, yamekusanywa maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 24,156,103.08** sawa na **asilimia 109.80** ya makadirio, ambayo yametokana na malipo ya kamisheni zinazotokana na makato ya bima kwa wanajeshi kwa Shirika la

Bima la Taifa (National Insurance Corporation - NIC). Fungu 39: JKT lilikusanya **Shilingi 64,403,000.00** sawa na **asilimia 100.00** zilizotokana na mauzo ya mazao ya kilimo, ikiwemo mboga mboga na matunda. Fungu 57: Wizara, limekusanya jumla ya **Shilingi 90,200,000.00** sawa na **asilimia 7,516.67.** Utofauti huu mkubwa umetokana na malipo ya deni la ukodishaji wa simu za *Zhong Xing Telecommunication Equipment* (ZTE). Haya yalikuwa malipo ya mara moja na hali hii haitarajiwi kujitokeza tena na kuathiri maduhuli yanayofuata. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa kwenye **Jedwali Na.1**.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025.**

| Fungu | Makadirio ya Mapato 2024/25 (Tsh) | Makusanyo Julai 2024 hadi Aprili 2025 (Tsh) | Makusanyo (%) |
|---|---:|---:|---:|
| 38 – NGOME | 22,000,000.00 | 24,156,103.08 | 109.80 |
| 39 – JKT | 64,403,000.00 | 64,403,000.00 | 100.00 |
| 57 – Wizara | 1,200,000.00 | 90,200,000.00 | 7,516.67 |
| **Jumla** | **87,603,000.00** | **178,759,103.08** | **204.06** |

**Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**Fedha Zilizoidhinishwa**

29. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,326,230,419,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika mafungu yake matatu ambayo ni Fungu 38: NGOME, Fungu 39: JKT na Fungu 57: Wizara**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,008,812,907,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 317,417,512,000.00** ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo. Fungu 38: NGOME liliidhinishiwa fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 2,491,439,934,000.00**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 48,867,636,000.00**; Fungu 39: JKT liliidhinishiwa fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 490,652,279,000.00**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 8,549,876,000.00**; Fungu 57: Wizara liliidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 26,720,694,000.00**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 260,000,000,000.00**. Muhtasari wa Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25**

| Fungu | Matumizi ya Kawaida (Tshs) | Matumizi ya Maendeleo (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 38 – NGOME | 2,491,439,934,000.00 | 48,867,636,000.00 | 2,540,307,570,000.00 |
| 39 – JKT | 490,652,279,000.00 | 8,549,876,000.00 | 499,202,155,000.00 |
| 57 – Wizara | 26,720,694,000.00 | 260,000,000,000.00 | 286,720,694,000.00 |
| **Jumla** | **3,008,812,907,000.00** | **317,417,512,000.00** | **3,326,230,419,000.00** |

**Fedha Zilizopokelewa Kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025.**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ni **Shilingi 2,605,257,552,583.97,** sawa na **asilimia 78.32** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,471,841,028,629.64** sawa na **asilimia 82.15** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 133,416,523,954.33** sawa na **asilimia 42.03** ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa Shughuli za Maendeleo. Katika kiasi hiki Fungu 38: NGOME limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 2,042,765,184,281.75** sawa na **asilimia 81.99**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 12,363,521,537.701** sawa na **asilimia 25.30**. Fungu 39: JKT limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 407,035,433,833.03** sawa na **asilimia 82.96**, na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 8,549,876,000.00** sawa na **asilimia 100**. Fungu 57: Wizara limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 22,040,410,514.86** sawa na **asilimia 82.48**, na

Shughuli za Maendeleo **Shilingi 112,503,126,416.63** sawa na **asilimia 43.27**. Muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika **Jedwali Na. 3**

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025**

| Fungu | Aina ya Matumizi | Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 | Mapokezi ya Fedha kuanzia Julai 2024 - Aprili 2025 | Asilimia (%) Bajeti Vs Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| | | (TZS) | (TZS) | |
| 38 - NGOME | Mishahara | 2,009,481,331,200.00 | 1,648,552,020,115.28 | 82.04 |
| | Chakula | 283,627,534,735.00 | 236,356,278,958.17 | 83.33 |
| | Posho msamaha wa kodi | 89,028,060,000.00 | 66,771,045,000.00 | 75.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 109,303,008,065.00 | 91,085,840,208.30 | 83.33 |
| | Maendeleo | 48,867,636,000.00 | 12,363,521,537.70 | 25.30 |
| | **Jumla ya Fungu** | **2,540,307,570,000.00** | **2,055,128,705,819.45** | 80.90 |
| 39 - JKT | Mishahara | 335,407,659,000.00 | 288,414,072,666.00 | 85.99 |
| | Chakula | 75,443,214,000.00 | 50,420,189,500.00 | 66.83 |
| | Posho msamaha wa kodi | 11,940,000,000.00 | 8,100,000,000.00 | 67.84 |
| | Matumizi Mengineyo | 46,861,406,000.00 | 39,101,171,667.03 | 83.44 |
| | Mafunzo ya Vijana Mujibu | 21,000,000,000.00 | 21,000,000,000.00 | 100.00 |
| | Maendeleo | 8,549,876,000.00 | 8,549,876,000.00 | 100.00 |
| | **Jumla ya Fungu** | **499,202,155,000.00** | **415,585,309,833.03** | 83.25 |
| 57 - WIZARA | Mishahara | 11,520,812,000.00 | 8,025,137,500.00 | 69.66 |
| | Matumizi Mengineyo | 15,199,882,000.00 | 14,015,273,014.86 | 92.21 |
| | Maendeleo | 260,000,000,000.00 | 112,503,126,416.63 | 43.27 |
| | **Jumla ya Fungu** | **286,720,694,000.00** | **134,543,536,931.49** | 46.92 |
| | **Jumla Kuu** | **3,326,230,419,000.00** | **2,605,257,552,583.97** | **78.32** |

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025, Fungu 57: Wizara imepokea uhamisho wa fedha (*Reallocation between votes*) kiasi cha **Shilingi 1,254,538,735,667.00** kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 1,189,270,693,916.00** zimetolewa kugharamia ununuzi wa zana na vifaa vya medani kwa matumizi ya JWTZ, na **Shilingi 65,268,041,751.06** kugharamia deni la kimkataba na hivyo kufanya jumla ya Bajeti ya Fedha za Maendeleo kuwa **Shilingi 1,514,538,735,667.00.**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepokea pia uhamisho wa fedha (*Reallocation between votes*) wenye jumla ya **Shilingi 103,092,029,422.93** kwa Fungu 38: NGOME kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa zana na vifaa, na hivyo kufanya jumla ya Fedha za Maendeleo kuwa **Shilingi 151,959,665,422.93**.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Fungu 38: NGOME imepokea uhamisho wa fedha (*Reallocation between votes*) wenye jumla ya **Shilingi 133,668,246,972.06** za Matumizi Mengineyo (Other Charges - OC) hivyo kufanya jumla ya Fedha za matumizi mengineyo kuwa **Shilingi 242,971,255,037.06**. Fedha hizo zimetumika kugharamia Operesheni Maalumu nchini Msumbiji, ununuzi wa mafuta ya zana na vifaa vilivyotumika kwa ajili ya zoezi la medani kati ya JWTZ na Jeshi la Ukombozi la Watu wa China, maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa,

malipo ya madeni ya matibabu kwa ajili ya maafisa na askari katika hospitali mbalimbali nchini, ununuzi wa mavazi, pamoja na kugharamia chakula cha Kuruti.

**Matumizi ya Fedha za Kawaida**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/25, zimetumika kwa shughuli zifuatazo:

a. Matunzo ya zana na vifaa vya Jeshi;

b. Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi kwa maafisa na askari katika Shule na Vyuo vya Kijeshi ndani na nje ya Nchi;

c. Kuwapatia Wanajeshi mafunzo ya awali na kuwaendeleza katika taaluma mbalimbali na uongozi;

d. Kuwapatia vijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya Kijeshi ukakamavu, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa, na stadi za kazi ili kuweza kujitegemea;

e. Kutoa huduma za afya na tiba kwa maafisa, askari, watumishi wa umma na familia zao, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, na wananchi wanaoishi karibu na vituo vya afya vya Jeshi;

f. Kutatua migogoro ya ardhi;

g. Kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika uokozi kwenye majanga mbalimbali, na kutekeleza na kulinda miradi ya kimkakati;

h. Kutoa stahili mbalimbali ikiwemo mishahara, malipo ya likizo kwa maafisa, askari na watumishi wa umma, kuwasafirisha wastaafu na mizigo yao, na lishe kwa wanaoishi na Virusi vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini;

i. Kuimarisha utawala bora kwa kutumia sheria za matumizi ya fedha na ununuzi, ambapo taarifa za ukaguzi na ununuzi zimekuwa zikiandaliwa na kuwasilishwa kwenye Mamlaka husika; na

j. Kuimarisha ushirikishwaji wa watumishi kupitia vikao mbalimbali ikiwa ni pamoja na Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya Maadili, na Kamati ya Ajira.

**Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi**

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi katika shule na vyuo vya kijeshi kwa wanajeshi. Vilevile, JWTZ imetoa mafunzo ya awali, na kuwaendeleza

wanajeshi katika taaluma mbalimbali za uongozi. Aidha, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kupeleka maafisa na askari nje ya nchi kwa ajili ya kupata mafunzo mbalimbali ya kijeshi, ambayo yameongeza weledi katika utendaji. Vilevile, katika kipindi husika JWTZ ilifanya zoezi la kijeshi la kutimiza Miaka 60 ya Jeshi, zoezi la *AMANI UMOJA* kwa kushirikiana na Jeshi la China na mazoezi mawili *JUSTIFIED ACCORD* na *CUTLASS EXPRESS* 2025 kwa kushirikiana na Jeshi la Marekani kwa kuzialika Nchi kumi na nne ikiwemo Comoros, Djibouti, Georgia, Kenya, Madagascar, Malawi, Marekani, Mauritius, Morocco, Msumbiji, Shelisheli, Somalia, Ufaransa na Ubelgiji. Vilevile, JWTZ kupitia Kamandi ya Jeshi la Wanamaji ilifanya zoezi la pamoja na Jeshi la Wanamaji kutoka Jamhuri ya India liitwalo Africa India Key Maritime Engagement (AIKEYME). Zoezi hilo lilishirikisha pia nchi nyingine tisa za Afrika ambazo ni Afrika Kusini, Comoros, Djibouti, Kenya, Mauritius, Madagascar, Msumbiji, Shelisheli na Uganda. Lengo la zoezi lilikuwa kuimarisha uwezo na kubadilishana maarifa katika kupambana na matishio ya kwenye maji (maritime) ikiwa ni pamoja na usafirishaji haramu wa binadamu, usafirishaji haramu wa silaha na dawa za kulevya. Mazoezi haya yalichangia katika kuimarisha na kuwajengea uwezo maafisa na askari wetu.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** ufanisi wa mazoezi na mafunzo haya, pamoja na mambo mengine hutegemea maeneo maalum yaliyotengwa kwa mazoezi husika. Naomba kupitia Bunge lako

Tukufu kutoa rai kwa wananchi kutovamia maeneo ya JWTZ, kwani kufanya hivyo ni kuhatarisha usalama wa maisha yao, kutokana na shughuli za kijeshi zinazofanyika katika maeneo hayo, ikiwemo mafunzo na mazoezi mbalimbali ambayo yanatumia risasi za moto, milipuko na zana zenye mionzi. Aidha, kufanya uvamizi katika maeneo hayo, ni kuhatarisha usalama wa Taifa, na kukwamisha shughuli muhimu za kuliweka tayari Jeshi letu kukabiliana na matishio yanayoweza kujitokeza.

**Matengenezo na Matunzo ya Zana na Mitambo**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kufanya matengenezo na matunzo ya zana na vifaa mbalimbali ili kuliimarisha Jeshi, ikiwemo; matengenezo na matunzo ya ndege vita na Helikopta, matengenezo na maboresho ya *RADAR*, matengenezo ya magari ya Deraya, na silaha mbalimbali, maboresho ya magati na vyelezo, matengenezo ya meli na boti. Vilevile, ukarabati wa mitambo na mashine umefanyika katika mashirika ya Mzinga na TATC – Nyumbu.

**Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa, stadi za kazi ili kuweza kujitegemea. Mafunzo haya yamefanyika kwa Mujibu wa Sheria na Kujitolea kwenye kambi mbalimbali za JKT.

Katika Mwaka wa Fedha 2024/25 mafunzo yamefanyika kupitia **Operesheni Miaka 60 ya Muungano,** ambapo jumla ya vijana **34,000** wa Mujibu wa Sheria walipatiwa mafunzo kwenye kambi mbalimbali za JKT. Kati yao wavulana ni **24,880** na wasichana ni **9,120**. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2024/25 yamefanyika pia Mafunzo kwa vijana wa Kujitolea kupitia Operesheni **Miaka 60 ya Muungano,** ambapo jumla ya vijana **12,000** wamepatiwa mafunzo. Kati yao wavulana ni **8,433** na wasichana ni **3,567**.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wahitimu wote wa Kidato cha Sita wanapata fursa ya kujiunga na mafunzo ya JKT, miundombinu ya kambi imeendelea kuboreshwa, ambapo hadi Mwaka 2025 JKT imefikia uwezo wa kuchukua vijana **60,000**. Aidha, Mpango uliopo ni kuendelea kuboresha miundombinu iliyopo na kufungua kambi mpya ili kulipa JKT uwezo wa kuchukua vijana **120,000** ifikapo Mwaka 2031, na kuwezesha wahitimu wote wa Kidato cha Sita kupata fursa ya kujiunga na JKT kwa Mujibu wa Sheria.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa Watanzania kwamba, mafunzo yanayotolewa kwa vijana wa JKT yameendelea kuwajengea uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, kuwapatia stadi za kazi katika nyanja mbalimbali na stadi za maisha ili wakimaliza mafunzo ya JKT waweze kurejea katika jamii wakiwa

raia wema wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa. Nitoe rai kwa vijana wote wanaopata fursa ya kupata mafunzo hayo, kuwa raia wema na kuzitumia stadi walizozipata kujiajiri na kujitegemea.

**Kilimo cha Kimkakati**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** kama sehemu ya kujitegemea, Wizara kupitia JKT imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kilimo (2019/2020 – 2024/2025) ambao umehuishwa kwa kuongeza muda wa utekelezaji mpaka kufikia Mwaka 2027/2028 na unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula, ili kuipunguzia Serikali gharama za kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na kuchangia katika usalama wa chakula kwa Taifa. Katika Msimu wa Kilimo 2023/2024, JKT kupitia Mkakati huo imezalisha kiasi cha **tani 3,222.4** za Mahindi na **tani 1,002.3** za Mpunga. Kati ya kiasi hicho, **tani 1,680** za Mahindi na **tani 1,002.3** za Mpunga zimetumika kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT, na **tani 1,542.4** za Mahindi zilizosalia zimechangia katika usalama wa chakula nchini. Aidha, Wizara kupitia JKT, imeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania katika uendelezaji wa teknolojia na utafiti wa kilimo wa uzalishaji wa miche ya michikichi na kahawa, pamoja na mbegu za Mpunga na Alizeti. Katika Msimu huu wa Kilimo zimezalishwa **tani 96** za Mpunga na **tani 94.32** za

Alizeti. Kiasi cha mbegu kilichozalishwa ni kwa ajili ya matumizi ya ndani na ziada kuuzwa kwa wananchi kwa bei nafuu.

### Mafunzo ya Jeshi la Akiba

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba. Mafunzo hayo hufanyika katika mikoa yote ya Tanzania na katika Mwaka wa Fedha 2024/25 jumla ya wananchi **14,803** walihitimu mafunzo hayo ambapo kati yao wanaume ni **12,203** na wanawake ni **2,600.** Mafunzo haya husimamiwa na Ofisi za Washauri wa Jeshi la Akiba katika Mikoa na Wilaya, kwa lengo la kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa masuala ya Ulinzi, na kuwajengea uwezo wahitimu katika kulitumikia Taifa lao. Niwapongeze wahitimu wote na kuwataka waendelee kuviishi viapo vyao vya kulinda raia, kutetea uhuru na uchumi wa nchi, pamoja na kutii sheria. Aidha, mafunzo haya hufanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Nitoe shukrani kwa ushirikiano huu na kuhimiza utengaji wa bajeti inayotakiwa kwa mafunzo haya muhimu.

### Maadhimisho ya miaka 60 ya JWTZ

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Tarehe 01 Septemba, 2024 JWTZ iliadhimisha miaka 60 tangu lilipoasisiwa, ambapo Sherehe za maadhimisho zilifanyika siku ya kilele kwa kufanya Gwaride

maalumu sambamba na Maonesho ya zana mbalimbali za kijeshi zilizopitishwa mbele ya Mgeni Rasmi, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Katika kipindi hiki cha miaka 60 kumekuwa na mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kulinda Muungano, Uhuru wa Taifa letu, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Katiba na mipaka ya Nchi yetu ya ardhini, kwenye maji na angani pamoja na kuzima matishio mbalimbali dhidi ya uvamizi wa Nchi yetu katika kipindi chote cha miaka 60. Kupitia Bunge lako Tukufu, nitoe pongezi kwa wanajeshi wetu kwa kazi kubwa wanayoendelea kufanya kwa kujituma na uzalendo wa hali ya juu. Aidha, ninamshukuru Rais na Amiri Jeshi Mkuu **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kazi kubwa ya kuliimarisha Jeshi letu na kuilinda Nchi yetu. Taifa salama na imara kabisa.

**Huduma za Afya na Tiba**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi husika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa huduma za tiba kwa maafisa, askari, watumishi wa umma, na familia zao pamoja na wananchi wanaoishi karibu na hospitali au vituo vya tiba vya Jeshi. Katika kuboresha huduma za afya, juhudi mbalimbali zimefanyika kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ikiwemo mashine za *Digitalized X-ray, Ultrasound, Magnetic Resonance Imaging (MRI), Computed Tomography Scan* (CT scan) katika hospitali za Jeshi

Lugalo, Mwanza, na Dodoma. Vilevile, JWTZ imeboresha upatikanaji wa huduma muhimu, ikiwemo usafishaji wa figo na uchunguzi wa matatizo ya moyo katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo. Pia, huduma katika hospitali za kanda na vituo vya tiba vikosini zimeendelea kuboreshwa kwa kupatiwa vifaa tiba na kuongezewa madaktari bingwa. Vilevile, matumizi ya Mfumo uliosimikwa katika hospitali zetu umewezesha kukusanya taarifa za wagonjwa, kufuatilia matibabu na maendeleo yao kimtandao. Taarifa hizo zinawezesha vituo kusomana kati yao na Kituo Kikuu (Data Centre), kuagiza madawa na kutuma taarifa Wizara ya Afya. Huduma ya Bima ya Afya Jeshini imeboreshwa kwa kuweka utaratibu wa kushirikiana na hospitali zisizo za kijeshi.

**Ushirikiano na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali zikiwemo, kutoa misaada wakati wa majanga na maafa ambapo, katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Wizara ilishiriki katika uokoaji Kariakoo, Dar es Salaam kufuatia kuporomoka kwa jengo; uokozi wakati wa mafuriko Rufiji na Morogoro, ujenzi wa nyumba za wafugaji Handeni Tanga, na ujenzi wa nyumba za waathirika wa maafa ya maporomoko ya matope Hanang'. Aidha, Wizara kupitia JWTZ imeweza, kushiriki katika utekelezaji na ulinzi wa miradi ya

kimkakati ikiwa ni pamoja na Reli ya Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway), vyanzo vya maji na umeme ikiwa ni pamoja na Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP), Mgodi wa *Tanzanite*, Bomba la Mafuta kati ya Tanzania na Uganda, Kivuko cha Busisi, Bandari, Mkongo wa Taifa, na maeneo ya viwanja vya ndege.

**Ushiriki katika Michezo ya Kitaifa na Kimataifa**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika Mwaka wa Fedha 2024/25 imeshiriki michezo mbalimbali ikiwemo SHIMIWI, iliyofanyika Mwezi Septemba hadi Oktoba 2024 mkoani Morogoro na michezo ya Mei Mosi, iliyofanyika Mwezi Aprili hadi Mei 2025 mkoani Singida. Vilevile, Shirika la Mzinga limeshiriki mashindano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA), yaliyofanyika jijini la Tanga Mwezi Novemba 2024. Katika mashindano hayo Shirika la Mzinga limeweza kushika nafasi ya pili kwa mshindi wa jumla katika michezo mbalimbali. Aidha, Wizara imeshika nafasi ya pili kwa mshindi wa jumla.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ na JKT imeshiriki katika michezo mbalimbali ndani na nje ya Nchi ikiwemo; Mashindano ya Michezo ya Majeshi kwa nchi za Afrika yaliyoandaliwa na Umoja wa Michezo ya Majeshi Barani Afrika yaliyofanyika mwezi Novemba 2024 Jijini Abuja Nchini Nigeria,

Mbio za Kimataifa za *Shenzhen Marathon* zilizofanyika nchini China mwezi Disemba 2024, Mashindano ya Mapinduzi ya Mpira wa Magongo yaliyofanyika Mwezi Februari 2025 Jijini Dar es Salaam, Mashindano ya Mbio za Nyika za *Half Marathon* zilizoandaliwa na Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani katika Michezo ya Majira ya Baridi (CISM Winter Games) yaliyofanyika Jijini Lucerne Nchini Uswizi mwezi Machi 2025, ambapo Timu Teule ya Riadha ya JWTZ ilikuwa mshindi wa kwanza na kupata Medali ya Dhahabu, Mashindano ya ubingwa wa mpira wa miguu kwa wachezaji wa kike chini ya miaka 17 (JKT Queens) yaliyofanyika Mwezi Januari 2025. Aidha, timu za majeshi zimechangia kwa kiwango kikubwa kutoa wachezaji katika Timu ya Taifa ya wanawake (Twiga Stars).

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika michezo hii na mashindano haya, wanamichezo wetu waliweza kupata ushindi na kuliletea Taifa letu medali na heshima. Napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza washindi wote walioshinda katika michezo hii. Vilevile, nawapongeza **Brigedia Jenerali Hassan Rashid Mabena** kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Mashindano ya AFCON yanayotarajiwa kufanyika hapa nchini Mwaka 2027, **Meja Mohamedi Haruna Kasui** aliyechaguliwa kuwa Rais wa Kamati ya Ufundi ya Mpira wa Kikapu wa Baraza la Michezo ya Majeshi ya Dunia (CISM) na kuwa Mtanzania na Mwafrika wa kwanza kushika nafasi hiyo tangu Mwaka 1948

Baraza lilipoanzishwa, **Sajini Alphonce Felix Simbu** aliyepata Medali ya Fedha katika Mbio Maarufu Duniani za Riadha (*Boston Marathon*)**,** nchini Marekani, **Koplo Magdalena Crispin Shauri** aliyepata Medali ya Dhahabu Mashindano ya Michezo ya Majeshi kwa nchi za Afrika yaliyoandaliwa na Umoja wa Michezo ya Majeshi Barani Afrika, **Praiveti Joseph Panga** aliyepata Medali ya Fedha katika Mashindano ya Mbio za Nyika za *Half Marathon*, **Praiveti King Lucas Mwajobaga** aliyeibuka na ubigwa katika mashindano ya Ngumi za kulipwa *Bantam weight*, **Praiveti Yusuph Changalawe** aliyeiwakilisha Tanzania katika mashindano ya Olimpiki na mshindi wa Mashindano ya Michezo ya Majeshi kwa Nchi za Afrika na **Timu ya JKT *Queens*** iliyoibuka na ubingwa katika Mashindano ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA). Niwapongeze viongozi wote wa JWTZ na JKT kwa kutoa uzito katika michezo na kuunga mkono maono ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuimarisha michezo. Niwapongeze pia, kwa kuboresha miundombinu ya Michezo na kuwezesha Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo kuwa miongoni mwa viwanja vitakavyotumika katika Michezo ya AFCON na CHAN.

49. ***Mheshimiwa Spika;*** kwa namna ya pekee, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa mchango wake uliowezesha wanamichezo wetu

kupata mafanikio makubwa ndani na nje ya Nchi na kuliletea sifa na heshima Taifa letu. Ushiriki huo umewezesha kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati ya Nchi yetu na nchi rafiki.

50. **Mapambano Dhidi ya Magonjwa Ambukizi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza**

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na Virusi vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza, kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe kwa watumishi wenye maambukizi ya VVU. Hatua hizi zinachukuliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Udhibiti VVU na UKIMWI. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imetoa elimu na kuhamasisha upimaji wa afya wa hiari na uchangiaji damu.

**Utawala Bora**

*52.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Wizara pamoja na taasisi zake imeendelea na jitihada mbalimbali ili kuimarisha Utawala Bora. Wizara na taasisi zake imezingatia sheria za matumizi ya fedha na ununuzi kwa kuhakikisha matumizi ya fedha na ununuzi hufanyika kwa ufanisi na kuzingatia thamani

ya fedha, na kaguzi zinafanyika ipasavyo. Wizara imepata Hati Safi ya Ukaguzi. Aidha, taarifa za kila Robo Mwaka huwasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Vilevile, semina mbalimbali kuhusu jinsi ya kupambana na kuzuia rushwa mahala pa kazi zimeendelea kutolewa kwa watumishi. Wizara imekuwa ikishirikisha watumishi katika kutoa maoni na ushauri kupitia vikao mbalimbali, hususan Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya Maadili, na Kamati ya Ajira. Aidha, Wizara inaendelea kutoa huduma bora kwa wateja kwa kuzingatia miongozo, kanuni na sheria mbalimbali za utawala bora.

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ, na JKT inamiliki maeneo ya kimkakati katika mikoa mbalimbali nchini, ambayo yametengwa maalum kwa matumizi ya kijeshi. Kama mnavyofahamu imekuwepo migogoro ya ardhi kati ya JWTZ na wananchi. Kupitia Mpango wa Wizara wa Kutatua Migogoro ya Ardhi wa Mwaka 2020/21 – 2024/25, Wizara imeendelea kutatua migogoro hiyo ambapo mpaka sasa imefanikiwa kutatua migogoro yote iliyotambuliwa kwa kuhuisha mipaka, kupima maeneo, kufanya uthamini, na kulipa fidia katika baadhi ya maeneo kwa wananchi wanaostahili. Maeneo ambayo mipaka imehuishwa, ardhi imepimwa na fidia imelipwa yameoneshwa katika **Jedwali Na. 4**. Wizara inaendelea na taratibu za kulipa fidia katika maeneo

ambayo bado wananchi hawajalipwa, maeneo hayo yanaonekana katika **Jedwali Na. 5.**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru **Mhe. Vincent Paul Mbogo (Mb.) Nkasi kusini, Mhe. Joseph Anania Tadayo (Mb.) Mwanga** na **Mhe. Antipas Zeno Mgugusi (Mb.) Malinyi** kwa uzalendo walioonyesha kuwezesha upatikanaji wa maeneo katika majimbo yao kwa ajili ya shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hususani JWTZ na JKT.

**Jedwali Na. 4: Maeneo yaliyofanyiwa uthamini na kulipwa fidia kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025**

| Na | Eneo | Mkoa | Kiasi kilicholipwa (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 1. | Fidia kwa wananchi katika maeneo manne yenye minara ambayo ni Msata, Ubena, Kiwangwa na Mandela. | Pwani | 8,838,170.00 |
| 2. | Fidia eneo la mnara kwa mwananchi 01 eneo la kijiji cha Moleti, Wilaya ya Kongwa. | Dodoma | 7,958,100.00 |
| 3. | Fidia eneo la mnara kwa Mwananchi 01 wa Ibihwa, Wilaya ya Bahi, Dodoma. | Dodoma | 10,883,460.00 |
| 4. | Fidia eneo la mnara Arumeru. | Arusha | 13,345,262.50 |
| 5. | Fidia eneo la mnara kwa wananchi wa Kijiji cha Kitefu, Usa river. | Arusha | 13,584,913.00 |
| 6. | Fidia katika eneo la mnara | Morogoro | 1,644,804.00 |

| Na | Eneo | Mkoa | Kiasi kilicholipwa (Tsh) |
|---|---|---|---|
| | Dakawa Mvomero. | | |
| 7. | Fidia eneo la mnara kwa wananchi wa eneo la Furwe, Wilaya ya Morogoro. | Morogoro | 757,613.50 |
| 8. | Fidia eneo la mnara kwa wananchi wa Ibuti Gairo. | Morogoro | 3,775,480.00 |
| 9. | Fidia ya eneo kwa wananchi 24 wa Mabama | Tabora | 363,003,000.00 |
| 10. | Fidia kwa maeneo matatu yatakapojengwa minara ambayo ni Mateke Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Gubilo na Wino katika Halmashauri ya Madaba. | Ruvuma | 4,025,701.20 |
| 11. | Fidia eneo la mnara Hedaru, Same. | Kilimanjaro | 7,628,000.00 |
| 12. | Fidia eneo la mnara Kiverenge, Mwanga. | Kilimanjaro | 7,246,010.00 |
| 13. | Fidia eneo la mnara Kitifu, Korogwe. | Tanga | 7,628,600.00 |
| 14. | Fidia eneo la minara 02 Kabuku na Kitumbi. | Tanga | 19,211,200.00 |
| 15. | Fidia eneo la minara 02 Mazinde na Buiko. | Tanga | 14,738,100.00 |
| 16. | Fidia eneo la mnara kwa wananchi wa eneo la kijiji cha Genge wilayani Muheza. | Tanga | 19,883,800.00 |
| 17. | Fidia ya ardhi maeneo manne yenye minara kwa wananchi katika Kata ya Yombo, Buguruni, Kigogo na Msigani | Dar es Salaam | 85,759,635.00 |

| Na | Eneo | Mkoa | Kiasi kilicholipwa (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 18. | Fidia ya ardhi katika eneo la mwananchi 01 Kijiji cha Kinyambi eneo la Nyamisugura, Wilaya ya Tarime. | Mara | 6,430,480.01 |
| 19. | Fidia ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa minara kwa wananchi wawili 02 katikavijiji vya Ikungi na Isuna 'A' katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi. | Singida | 22,756,670.00 |
| 20. | Fidia ya ardhi kwa wananchi 02 katika Kijiji Gurugu. | Singida | 11,680,416.00 |
| 21. | Fidia ardhi kwa wananchi wa eneo la Mseko, Wilaya ya Ilamba | Singida | 10,970,130.00 |
| 22. | Fidia ya ardhi katika eneo Kikosi cha 122 Rejimenti Nhobola Nzega na eneo la Ipazi/Kitangiri. | Tabora | 2,196,360,394.00 |
| 23. | Fidia katika eneo la Senje Msalato Dayosisi ya *Central Tanganyika* | Dodoma | 2,093,853,977.00 |
| 24. | Fidia kwa ajili ya ununuzi wa Shamba na. 104 eneo la Nduruma, Duluti. | Arusha | 7,908,000,000.00 |
| 25. | Malipo ya fidia katika eneo la Shule ya Kijeshi ya Mawasiliano (SKM) Rufiji | Pwani | 230,958,981.00 |
| 26. | Malipo ya fidia katika eneo la 977 Regt Losirway Moshono | Arusha | 2,278,836,961.06 |

**Jedwali Na. 5: Maeneo yaliyofanyiwa uthamini Mwaka 2020/21 hadi 2024/25, ambayo bado fidia haijalipwa (Maombi yamewasilishwa Hazina kwa Malipo)**

| Na. | Eneo | Mkoa | Fidia (TZS) | Kitabu kilipo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 191Regt Bomani Kibasila Kisarawe | Pwani | 2,520,249,865.00 | HAZINA |
| 2. | Chimlata | Dodoma | 459,725,310.00 | HAZINA |
| 3. | Senje Msalato | Dodoma | 1,073,498,023.00 | HAZINA |
| 4. | AFS/601KJ Kiseke Ilemela | Mwanza | 354,795,000.00 | HAZINA |
| 5. | 977 Regt Olumitu Losirway | Arusha | 3,016,902,317.28 | HAZINA |
| 6. | Mtabila JKT 825KJ | Kigoma | 1,312,755,175.49 | HAZINA |
| 7. | SMH Pangawe Vol 1 | Morogoro | 84,416,152.00 | HAZINA |
| 8. | SMH Pangawe Vol 2 | Morogoro | 335,868,372.25 | HAZINA |
| 9. | SMH Pangawe Ngong'olo | Morogoro | 2,975,154,589.99 | HAZINA |
| 10. | 601KJ Ngerengere | Morogoro | 147,342,403.45 | HAZINA |
| 11. | Itaka Sasenga Village | Songwe | 3,491,271,800.00 | HAZINA |
| 12. | Itaka Mboji Village | Songwe | 74,358,600.00 | HAZINA |
| 13. | Itaka Itewe Village | Songwe | 2,150,311,800.00 | HAZINA |
| 14. | 11KJ Ubago (222 PAPs) | Zanzibar | 13,163,218,538.50 | HAZINA |
| 15. | 141Regt Dunga (272 PAPs) | Zanzibar | 8,740,014,265.75 | HAZINA |
| | **JUMLA** | | **39,899,882,212.71** | |

## Utunzaji wa Mazingira

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuchukua hatua mahususi ili kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi. Kupitia taasisi zake, Wizara imeendelea na utunzaji wa mazingira katika maeneo yake yenye miti ya asili, kwa kulinda maeneo hayo yasivamiwe kwa shughuli za kijamii, na kuendelea kupanda miti mipya. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Wizara na Taasisi zake imeweza kupanda miti mipya katika maeneo yenye ukubwa wa **ekari 964.9**. Vilevile, Wizara imeendelea na utunzaji wa fukwe katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi. Aidha, maeneo yote ya Jeshi yana zuio la ukataji miti, kuchoma mkaa na kulisha mifugo. Napenda nitoe wito kwa wananchi wote kuzingatia zuio la ukataji miti na kuchoma mkaa katika maeneo ya Jeshi.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu matumizi ya Nishati safi JWTZ na kambi zake zinazolisha zaidi ya watu 100 yamefikia 92% ya matumizi ya Nishati Safi ya kupikia, JKT imefikia 98%, Shirika la Mzinga 98%, na Shirika la TATC - Nyumbu 98%. Aidha, matumizi ya Nishati Safi yamekuwa na matokeo makubwa ikiwa ni pamoja na kuokoa kiasi cha **Shilingi 2,325,000,000.00,** kutumia muda mchache wa kuandaa chakula na muda kutumika kwa tija katika

mafunzo ya vijana, kulinda afya za wapishi kwa magonjwa yanayosababishwa na moshi unaotokana na nishati chafu, na matumizi ya nishati safi yamekuwa shamba darasa kwa vijana wanapokuwa kwenye mafunzo ya JKT, ili baadae waweze kutumia ujuzi huo katika shughuli za kiuchumi na kujitegemea.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu napenda nitoe shukrani kwa ushirikiano mkubwa kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika kuisaidia Wizara kutekeleza shughuli za utunzaji wa Mazingira.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Mashirika yaliyo chini ya Wizara ambayo ni TATC - Nyumbu, Mzinga na SUMAJKT yameendelea na uzalishaji wa bidhaa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na njia za kisasa za kusafisha maji yenye kemikali yanayotoka viwandani. Vilevile, viwanda vimeendelea na utaratibu wa kuwapa wafanyakazi wake vifaa kinga ili kuzuia madhara yatokanayo na kelele na kemikali.

**Matumizi ya Fedha za Maendeleo**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara imeweza kutumia Fedha za Maendeleo kutekeleza yafuatayo:

a. Kugharamia malipo ya mikataba mbalimbali ya ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya JWTZ. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imezingatia ushauri wa Bunge lako Tukufu wa kwenda na mahitaji ya teknolojia ya kisasa, na kuimarisha utafiti;
b. Kugharamia mikataba ya mafunzo na matengenezo ya ndege vita na *Helicopters*, pamoja na mafunzo ya marubani;
c. Kugharamia utafiti na uhuishaji wa silaha, zana na vifaa jeshini;
d. Kugharamia uboreshaji wa minara ya Mfumo wa Mawasiliano Salama, huduma ya ulinzi wa minara, na ulipaji wa huduma ya umeme kwenye minara;
e. Kuendeleza na kujenga miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na maghala ya kuhifadhia silaha, Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (MMUT) Kikombo, Ujenzi wa Hospitali Kuu ya Rufaa ya Jeshi Msalato – Dodoma, makazi ya washiriki wa kozi Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), Bweni la askari kapera wanawake Monduli (TMA), Makao

Makuu ya Kamandi ya Jeshi la Akiba, na Shule ya Polisi Jeshi;

f. Kugharamia ununuzi wa Mazao ya Msingi;

g. Kugharamia shughuli za utafiti wa viwanda vya Kijeshi kupitia Shirika la Nyumbu (TATC) na Mzinga;

h. Ujenzi wa mahanga ya vijana katika kambi mbalimbali ya JKT, ujenzi wa Kiteule cha Tanganyika ambacho kinatarajiwa kuwa kikosi kipya cha Jeshi la Kujenga Taifa, na kuendeleza ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika kikosi cha Chita; na

i. Kugharamia shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini ya miradi.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa Hospitali Kuu ya Rufaa ya Jeshi Msalato – Dodoma yenye viwango vya Umoja wa Mataifa unaendelea kwa kushirikiana na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, ambapo awamu ya kwanza imekamilika na kukabidhiwa rasmi tarehe 03 Aprili, 2025. Kazi zilizokamilika ni zifuatazo:

a. Ujenzi wa majengo ya Hospitali ambao umekamilika kwa asilimi 100; na

b. Ujenzi wa awamu ya pili na ya tatu unaohusisha maeneo ya kutolea huduma za matibabu na kulaza wagonjwa 150, ambao umefikia asilimia 95.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Mpango wa kujenga Hospitali hii ni wa awamu tano (5), ambapo awamu ya nne itahusisha ununuzi wa vifaa tiba (Medical Equipment) na samani za maofisini pamoja na kuongeza uwezo wa kulaza wagonjwa kufikia **450.** Utekelezaji wa awamu ya nne utagharimu jumla ya **Shilingi 55,657,451,967.09** kwa kukamilisha ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto utakaogharimu **Shilingi 15,133,545,600.00**; ujenzi wa *Diagnostic Centre* utakaogharimu **Shilingi 14,334,604,373.00**; ujenzi wa wodi za wagonjwa utakaogharimu **Shilingi 6,965,686,021.09**; ununuzi wa samani za Ofisi utakaogharimu **Shilingi 4,443,933,100.00**; na ununuzi wa vifaa tiba utakaogharimu **Shilingi 14,779,682,873.00.**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Shirika la TATC - Nyumbu, Shirika la Mzinga, na SUMAJKT imeendelea kutekeleza majukumu yake ifuatavyo:

### *Tanzania Automotive Technology Centre* (TATC) – Nyumbu

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, Shirika la Nyumbu limeendelea kutekeleza majukumu ya msingi ifuatavyo:

a. Kufanya utafiti katika teknolojia kwa kuhawilisha teknolojia zilizopo duniani kwa ajili ya kutanzua matatizo yaliyopo katika sekta za ulinzi na usalama, usafirishaji, kilimo na viwanda;

b. Kufanya usanifu wa magari na mitambo kwa ajili ya kuyazalisha nchini;

c. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa viwanda nchini, katika nyanja za uhandisi mitambo, usanifu na uzalishaji;

d. Kufanya utafiti wa malighafi kwa ajili ya matumizi katika uhandisi mitambo, hususani katika teknolojia ya kukalibu vyuma (Foundry engineering);

e. Kutoa mafunzo ya teknolojia za kisasa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu hapa nchini; na

f. Kufanya uhakiki wa ubora wa mitambo na zana za kijeshi zinazonunuliwa na Wizara ya Ulinzi na JKT.

64. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu hayo, TATC - Nyumbu ina Mpango wa Miaka Kumi wa Kuliimarisha Shirika, ambao katika Mwaka wa Fedha 2024/25, uliidhinishiwa

jumla ya **Shilingi 15,575,090,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Mpango huo. Hadi kufikia Aprili 2025, Shirika limepokea jumla ya **Shilingi 5,000,000,000.00** sawa na **asilimia 32.10** ya kiasi kilichoidhinishwa. Fedha hizo zimetumika kuanzisha Karakana Kuu ya kukalibu chuma (Heavy Duty Foundry Plant) kwa ajili ya kuzalisha vipuri vya magari, zana za kilimo na viwanda.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, ili kuendeleza viwanda vya kijeshi Shirika la Nyumbu linaendelea na limekamilisha taratibu za kuingia ubia kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha magari na kampuni ya *STREIT Group* kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Manufaa yatakayopatikana kutokana na ubia huu wa kimkakati ni kuongeza mtaji, kuongeza ajira, kupata teknolojia na kuimarisha uwezo wa kuunda magari ya Deraya na kiraia.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, TATC - Nyumbu imeweza pia kutekeleza shughuli zifuatazo kwa kutumia rasilimali za ndani:

a. Kufanya utafiti na kuzalisha vipuri mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya viwandani, migodini pamoja na uzalishaji wa breki za treni kwa ajili ya Shirika la Reli la Tanzania (TRC);
b. Kufanya maboresho ya magari ya Wizara ya Afya kwa kufunga vifaa tiba ili yawe magari ya kubebea wagonjwa;

c. Ukarabati wa pampu za maji na vipuri vya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA);
d. Uundaji wa majiko yanayokokotwa na gari (*Mobile field Kitchen*); na
e. Uundaji wa vitanda vya chuma na vifaa mbalimbali kwa ajili ya JWTZ.

**Shirika la Mzinga**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mzinga limeendelea kutekeleza majukumu ya msingi ifuatavyo:

a. Kuzalisha Mazao ya Msingi kwa ajili ya matumizi ya Jeshi na vyombo vya usalama;
b. Kufanya tafiti mbalimbali za kijeshi na kiraia;
c. Kufanya Ukarabati wa vifaa na mitambo ya kijeshi na kiraia; na
d. Kutekeleza majukumu muhimu kwa maendeleo ya Shirika na Taifa kwa ujumla.

68. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza majukumu ya msingi, Shirika la Mzinga kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 liliidhinishiwa **Shilingi 6,000,000,000.00,** ambapo hadi kufikia Aprili 2025 Shirika limepokea **Shilingi 2,000,000,000.00** sawa na **asilimia 33.33** kwa ajili ya ununuzi wa zana na mashine zitakazotumika katika uzalishaji wa mazao ya msingi.

69. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na shughuli za msingi, Shirika limeendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani ifuatavyo:

a. Kuendelea na uzalishaji wa mazao ya msingi kwa ajili ya matumizi ya JWTZ na vyombo vya usalama;
b. Kufanya ukarabati wa silaha ndogo za JWTZ na vyombo vya usalama;
c. Kuendelea na uzalishaji wa vipuri vinavyotumika katika mashine za uzalishaji wa Zao la Msingi;
d. Kuendelea na uzalishaji wa mabomu baridi ya kufukuza tembo kwenye makazi yaliyopo karibu na hifadhi. Hadi kufikia Aprili 2025 mabomu 11,817 yamezalishwa. Aidha, kwa ushirikiano na TAWIRI, utengenezaji wa kifaa mahsusi cha kurushia bomu baridi umekamilika. Kifaa hicho kitaongeza ufanisi na kupunguza madhara kwa watumiaji wa mabomu hayo;
e. Kuendelea kutoa huduma ya ununuzi na uuzaji wa silaha ndogo zinazotumiwa kwa ajili ya ulinzi binafsi;
f. Kuboresha Hospitali ya Mzinga na kutoa huduma za afya zinazotolewa ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma za viungo bandia;
g. Kuendelea na shughuli za ujenzi wa majengo kupitia Kampuni Tanzu ya Mzinga (Mzinga Holding Company Limited); na

h. Kuendelea kutoa huduma mbalimbali ikiwemo Huduma ya kumbi za mikutano kupitia Magadu Club na utoaji wa mafunzo ya stadi za kazi kupitia Chuo cha Ufundi Stadi Mzinga.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika jitihada za kuendelea kujiimarisha katika viwanda vya kijeshi, Wizara kupitia Shirika la Mzinga inaendelea na maandalizi ya kuanzisha Kiwanda kipya cha uzalishaji wa mazao ya msingi (Mzinga II). Kiwanda hiki kitaliwezesha Shirika kuzalisha kwa kutumia teknolojia ya kisasa, na hivyo kuongeza ufanisi, na upatikanaji wa uhakika wa mazao ya msingi kwa matumizi ya ndani na ziada kuuzwa nje ya Nchi na kuongeza mapato ya Shirika na Serikali, hususan fedha za kigeni.

**Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) lilianzishwa kwa madhumuni makuu mawili ifuatavyo:

a. Kuchangia gharama katika kuendesha shughuli za malezi ya vijana wa JKT; na
b. Kufanya uzalishaji wenye tija na hivyo kuchangia katika uchumi wa Taifa.

**Kuchangia gharama katika kuendesha shughuli za malezi ya vijana**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika katika kutekeleza lengo lake la kuchangia gharama za uendeshaji wa shughuli za malezi ya vijana wa JKT, Shirika limetekeleza yafuatayo:

a. Kukarabati miundombinu mbalimbali katika kambi za JKT pale inapohitajika;

b. Kulipatia JKT baadhi ya mashamba yake ili yatumike kama mashamba darasa kwa vijana wa JKT;

c. Shirika kuendelea kutoa mitambo na magari katika Skimu ya Umwagiliaji Chita na maeneo mbalimbali ya Kilimo Mkakati;

d. Miradi ya Shirika kuendelea kutumika kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vijana wanaojitolea ndani ya JKT; na

e. Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 limepanga kujenga vyoo vitatu (3) na mabweni kumi na nne (14) yenye uwezo wa kuchukua vijana **1,120** ambayo yatagharimu jumla ya **Shilingi 1,242,000,000.00.**

**Uzalishaji wenye tija na hivyo kuchangia katika uchumi wa Taifa**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea na shughuli za kiuchumi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta za ujenzi, viwanda, kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara na huduma. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika limetoa gawio la **Shilingi 1,034,550,000.00** kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali (HAZINA).

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Shirika limeimarisha ulinzi wa kimkakati kupitia Kampuni yake tanzu ya Ulinzi ya *SUMAJKT GUARD Ltd*, ambapo hadi sasa limeanza kutoa huduma ya ulinzi katika vituo vya Treni ya Kisasa (SGR), na Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), na katika Taasisi mbalimbali za Serikali.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, SUMAJKT imepokea jumla ya **Shilingi 3,080,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Mafanikio haya makubwa niliyoeleza katika Hotuba hii yametokana na juhudi za dhati za **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu za kuimarisha Wizara ya Ulinzi na JKT na Taasisi zake, na kuimarisha ulinzi na kusimamia ulinzi na amani ya Taifa letu.

## F. USHIRIKIANO WA KIULINZI NA KIMATAIFA

### Ushirikiano na Nchi nyingine

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia taasisi zake, ikiwa ni pamoja na JWTZ imeendelea kushirikiana na nchi rafiki katika masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali, ikiwemo mafunzo, mazoezi, misaada ya kitaalamu, zana na vifaa. Vilevile, ushirikiano umeimarishwa na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika mafunzo, mazoezi, ubadilishanaji wataalamu, na operesheni mbalimbali. Pia, JWTZ inaendelea kushirikiana na nchi rafiki katika mafunzo kwa maafisa na askari.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Nchi hizo rafiki ni pamoja na Afrika Kusini, Angola, Algeria, Brazil, Bangladesh, Botswana, Burundi, Canada, Comoros, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israel, Jamhuri ya Watu wa China, Jordan, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Nigeria, Oman, Kuwait, Pakistan, Rwanda, Sri Lanka, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

## Mafunzo ya Usalama na Stratejia

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi - Tanzania (National Defence College - Tanzania) imeendelea kutoa mafunzo ya Ulinzi, Usalama, na Stratejia kwa maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na maafisa waandamizi katika utumishi wa umma. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25 washiriki 61 wanahudhuria kozi ndefu, na washiriki 150 wamehudhuria kozi fupi ikilinganishwa na washiriki 53 wa kozi ndefu na washiriki 187 wa kozi fupi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Faida ya mafunzo haya kwa washiriki wa kozi ni kuwawezesha kupata maarifa juu ya ulinzi na usalama wa Taifa, na masuala ya ulinzi na usalama, kisera na kistrategia.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo haya yanahusisha pia washiriki toka nchi rafiki, ambapo katika kipindi husika Chuo kimetoa mafunzo kwa washiriki kutoka nchi za Afrika Kusini, Burundi, Eswatini, Ethiopia, India, Kenya, Malawi, Misri, Namibia, Nigeria, Rwanda, Sierra Leone, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

## Ushiriki wa JWTZ katika Shughuli za Ulinzi wa Amani

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda katika operesheni za ulinzi wa amani. Kwa sasa, JWTZ limeendelea kuwa na vikosi vya ulinzi wa amani katika nchi za Jamhuri ya

Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Lebanon chini ya Misheni za Umoja wa Mataifa. Vilevile, Wizara kupitia JWTZ ilishiriki katika Misheni ya Amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC Mission in DRC - SAMIDRC) ambayo ilimaliza muda wake mwezi Machi 2025, baada ya Wakuu wa nchi za SADC kukubaliana kuhitimisha Misheni hii ili kutoa nafasi kwa majadiliano ya amani. Pia, Wizara kupitia JWTZ inao maafisa wanadhimu na makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa JWTZ katika operesheni za Ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Mataifa na Kikanda, umeiwezesha Nchi yetu kujenga uwezo, kuimarisha diplomasia ya ulinzi, na kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa na jumuiya za kikanda ya kushiriki katika ulinzi wa amani kimataifa na kikanda.

## G. MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

83. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelenga kutekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia Dira na Dhima ya Wizara, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa

Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Mpango Mkakati wa Wizara na Taasisi zake kwa kuongozwa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 ifuatavyo:

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli**

85. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu, ambapo Fungu 38: NGOME linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39: JKT linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 64,403,000.00,** na Fungu 57: Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 1,200,000.00** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.**

**Jedwali Na. 6: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/26**

| Na. | Fungu | (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | 38 – NGOME | 22,000,000.00 |
| 2. | 39 – JKT | 64,403,000.00 |
| 3. | 57 – Wizara | 1,200,000.00 |

| | Jumla | 87,603,000.00 |
|---|---|---|

**Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

86. ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shughuli za Maendeleo ikiwa na jumla ya **Shilingi 3,645,912,947,000.00** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,327,115,385,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 318,797,562,000.00** ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo. Fungu 38: NGOME inatarajia kutengewa kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 2,733,729,204,000.00,** na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 48,867,636,000.00**; Fungu 39: JKT inatarajia kutengewa kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 567,023,845,000.00** na Shughuli za Maendeleo **Shilingi 9,929,926,000.00**; na Fungu 57: Wizara inatarajia kutengewa kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 26,362,336,000.00,** na Shughuli za maendeleo **Shilingi 260,000,000,000.00**. Mchanganuo umeainishwa katika **Jedwali Na. 7.**

**Jedwali Na. 7: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26**

| Na | Fungu | Matumizi ya Kawaida (Tshs) | Matumizi ya Maendeleo (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 38 -NGOME | 2,733,729,204,000.00 | 48,867,636,000.00 | 2,782,596,840,000.00 |
| 2 | 39 - JKT | 567,023,845,000.00 | 9,929,926,000.00 | 576,953,711,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 57 - Wizara | 26,362,336,000.00 | 260,000,000,000.00 | 286,362,336,000.00 |
| | **Jumla Kuu** | **3,327,115,385,000.00** | **318,797,562,000.00** | **3,645,912,947,000.00** |

87. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2025/26 zitazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

a. Kuendelea kuliimarisha Jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa na rasilimali watu;

b. Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi ikiwemo stahili, makazi, mafunzo, matengenezo ya vifaa, na huduma bora za afya;

c. Kuendelea kuimarisha miundombinu katika kambi, vikosi na shule za Jeshi;

d. Kuendelea kuimarisha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi watakaopata mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, na stadi za kazi kwa vijana wa Mujibu wa Sheria, na wa Kujitolea;

e. Kuendelea kuimarisha Jeshi la Akiba;

f. Kuendelea kulinda miradi ya kimkakati kwa maslahi mapana ya Taifa, na kushirikiana na mamlaka za kiraia kadri inavyohitajika;

g. Kuimarisha mashirika na taasisi za utafiti wa masuala ya kijeshi, kuimarisha viwanda katika Sekta ya Ulinzi (Defence Industries) na kuanzisha viwanda vipya kwa kushirikiana na Sekta Binafsi;

h. Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), jumuiya za kikanda, na nchi mbalimbali na hivyo kuimarisha Diplomasia ya Ulinzi, na maeneo mengine ya kimkakati;

i. Kuendelea kutoa mafunzo ya Ulinzi na Stratejia; na

j. Kuendelea kuimarisha mifumo ya utawala bora na huduma kwa watumishi.

## H. SHUKRANI

88. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijahitimisha Hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipatia, kazi kubwa wanayoifanya, na michango yao madhubuti iliyowezesha kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/25 kwa mafanikio na kwa ushirikiano mkubwa katika kutayarisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 ninayowasilisha. Napenda kumshukuru **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe,** Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Jenerali Jacob John Mkunda,** Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, **Luteni Jenerali Salum Haji Othman,** Mnadhimu Mkuu

wa Jeshi, **Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele,** Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Wakuu wa Kamandi wote**,** Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Matawi, Wakuu wa Vyuo, Shule na Vikosi vya Jeshi. Vilevile, nawashukuru maafisa, askari na watumishi wa umma wote kwa ushirikiano wanaonipatia. Mafanikio tuliyopata ni kutokana na bidii, nidhamu, uhodari na kujituma kwao. Mwenyezi Mungu awabariki na muendelee kulilinda Taifa letu.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa serikali za nchi mbalimbali na washirika wa maendeleo kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara ninayoiongoza, ikiwa ni pamoja na; Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, Canada, India, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Ufaransa, Ujerumani na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki katika shughuli zetu za ulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Angola, Afrika Kusini, Algeria, Bangladesh, Burundi, Jamhuri ya Czech, Ethiopia, Finland, Ghana, Hispania, Indonesia, Israel, Jordan, Kenya, Msumbiji, Kuwait, Malawi, Misri, Morocco, Nigeria, Oman, Pakistan, Rwanda, Serbia, Sri Lanka, Sweden, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuzishukuru Wizara na Taasisi zote, na wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Wizara ya Ulinzi na JKT na taasisi zake katika ulinzi wa Nchi yetu. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa letu.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Niwatakie nyote mafanikio katika uchaguzi mkuu, na niendelee kutoa wito kwa watanzania wote kujitokeza na kutumia haki yao ya kikatiba kushiriki ipasavyo katika uchaguzi mkuu na kufanya uchaguzi wa viongozi sahihi watakaoendelea kudumisha amani, utulivu na maendeleo ya Taifa letu. Hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni ***www.modans.go.tz***.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu na upendo wao mkubwa kwangu unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa utulivu na kujiamini.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee namshukuru **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kuniteua katika nafasi hii adhimu, na kwa uongozi wake mahiri, maono yake mapana, na kwa kuhakikisha kuwa Wizara na Taasisi zake tunaweza kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi, na Nchi yetu inaendelea kuwa imara na yenye amani na utulivu.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara ya Ulinzi na JKT na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 3,645,912,947,000.00** kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,327,115,385,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 318,797,562,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja.